# SEHEMU A: KISWAHILI

***Soma kifungu kisha ujaze mapengo.***

Tuliketi __1__ kupumzika baada ya kula __2__ chetu usiku huo. Siku __3__ tulikuwa na shughuli __4__. Tulipiga __5__ tukajadili __6__ mbali mbali kama siasa, uchumi na biashara. Tuliamua kupanga mipango ya __7__ maonyesho ya kilimo. Tulijua wazi __8__ kufaulu katika __9__ bila kupata mafunzo ya ukulima bora.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. maliwatoni | B. hawamamuni | C. sebuleni | D. kizimbani |
| 2. | A. kilalio | B. kishuka | C. mlo | D. shibe |
| 3. | A. huyo | B. huo | C. hii | D. hiyo |
| 4. | A. mingi | B. nyingi | C. kingi | D. vingi |
| 5. | A. debe | B. siahi | C. soga | D. doria |
| 6. | A. masuala | B. maswali | C. masala | D. masila |
| 7. | A. kudoea | B. kudhuru | C. kuduru | D. kuzuru |
| 8. | A. hatungeweza | B. tusingeweza | C. tungeweza | D. tusingeliweza |
| 9. | A. zaraa | B. biashara | C. siasa | D. uchumi |

Siku __10__ tuliamka mapema. Tulielekea kwenye __11__ ya magari na kuabiri gari. Tulimwomba utingo __12__ kwenye lango la maonyesho kwa kuwa hatukujua sehemu ile. Tulisafiri salama __13__. Utingo alitufaa. Tulishuka na kuenda moja kwa moja hadi langoni. Tulilipa __14__ na kuruhusiwa kuingia. Tulijifunza mengi na kufaidika. Kwa kweli mtembezi hula __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. inayofuata | B. iliyofuata | C. uliyofuata | D. iliyofuata |
| 11. | A. kituo | B. stani | C. maegesho | D. kiwanda |
| 12. | A. atushushe | B. atushushie | C. atushukishe | D. ashushe |
| 13. | A. salimini | B. salamani | C. salamini | D. salimina |
| 14. | A. nauli | B. masrufu | C. ridhaa | D. kiingilio |
| 15. | A. matembezi yake | safari yake | C. miguu yake | D. mali yake |



Test compiled by Schools Net Kenya, Term 1, 2016 | Available online at www.schoolsnetkenya.com
Contact details: E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 0711882227

***Kuanzia swali la 16 hadi 30 jibu kulingana na maagizo***

16. Ni kundi lipi ambalo lina vielezi pekee?
    A. Sana, jana, vizuri, waziwazi
    B. Mzuri, cheupe, virefu, pana
    C. Barabara, sahani, gari, shati
    D. Piga, cheka, lima, winda

17. Chagua sentensi ambayo si sahihi
    A. Chai inywewayo ni hii
    B. Nyasi ile itamea tena
    C. Mawaridi yote hunyauka
    D. Kichwani pake pana doa

18. Ni mpangilio upi unaonyesha sehemu za utawala kuanzia iliyo kubwa hadi iliyo ndogo?
    A. Kata, tarafa, wilaya, mkoa
    B. Wilaya, mtaa, kijiji, kata
    C. Wilaya, tarafa, kata, kijiji
    D. Mkoa, wilaya, kata, tarafa

19. ***Teua kivumishi cha pekee katika sentensi ifuatayo***
    Jasho jingi lilimtiririka usoni pake
    A. usoni B. jasho
    C. pake D. jingi

20. Mjomba wangu huniita ____
    A. mjombake B. ami yake
    C. mpwa wake D. mwamu wake

21. ***Andika kinyume cha:-***
    Msichana yule amewekwa kimada
    A. Mvulana yule amewekwa kimada
    B. Mvulana yule hajawekwa kimada
    C. Msichana yule amewekwa rumenya
    D. Mvulana yule amewekwa rumenya

22. Mtu anapolalia mgongo katika mapumziko tunasema amelala ____
    A. kifudifudi B. tani
    C. pono D. mang'amung'amu

23. Neno 'kwenye' limetumikaje katika sentensi?
    Watoto wanacheza kwenye uwanja
    A. kivumishi cha pekee B. kiunganishi
    C. kiwakilishi D. kihusishi

24. ***Andika sentensi ifuatayo kwa wingi:-***
    Upo wako upo katika jahazi lile
    A. Zipo zenu zipo katika majahazi yale
    B. Nyupo zenu zipo katika majahazi yale
    C. Upo zao zipo katika majahazi yale
    D. Nyupo zenu zipo katika jahazi zile

25. ***Kanusha sentensi ifuatayo:-***
    Nyanya angenishauri ningebadilisha tabia
    A. Nyanya asingelinishauri nisingelibadilisha tabia
    B. Nyanya asingalinishauri nisingalibadilisha tabia
    C. Nyanya hasingenishauri nisingebadilisha tabia
    D. Nyanya asingenishauri nisingebadilisha tabia

26. Kata ni kugawanya kitu kwa kutumia kitu chenye makali kama kisu. Aidha kata ni ____
    A. kutokubali jambo fulani
    B. nafasi isiyo upande huu au ule
    C. chombo cha kuchotea au kunywea maji
    D. kufanya mtu asitende jambo

27. Ni ipi ambayo ni nomino ambata sahihi?
    A. Sukaringuru B. Mtambaapaka
    C. Kidakamchuzi D. Kibiritingoma

28. Fatuma alimpiga Asha naye Asha akampiga Fatuma kwa hivyo ____
    A. walipigwa B. walipigana
    C. walipigiana D. walipigishwa

29. ***Tumia tanakali sahihi***
    Fenesi lilianguka matopeni ____________
    A. chumbwi B. chubwi
    C. tapwi D. tabwi

30. ***Tumia nomino za makundi kwa usahihi***
    Tarishi alibeba ______ cha barua na ______ cha funguo alipotoka posta
    A. kifurushi, kifungu B. kicha, kipeto
    C. kidani, kitita D. kipeto, kicha

***Soma habari ifuatayo kisha uchague majibu ya sawa zaidi ya maswali 31 hadi 40.***

Mioto inayotokea katika miji mbalimbali nchini, hasa Nairobi ina walakini. Mioto yenyewe aghalabu hutokea katika mitaa ya mabanda ambako watu wamesongamana. Jambo la kustaajabisha ni kwamba sehemu zinazotokea mioto huwa kuna mnyakuzi wa ardhi ambaye ana hamu ya kutaka watu hao kuondoka ili ajenge ghorofa zake. Lakini wenyeji huwa wamekataa katakata.

Ndiposa kukaanza kutafutwa hila za kuanzisha moto na mwisho kisingizio cha moto hupatikana eti stovu ilisahauliwa haikuzimwa na mambo kama hayo.

Wanyakuzi ni wanyakuzi. Wao hufanya juu chini mpaka lao walipate bila ya kujali mateso ambayo watu wengine wangeyapata. Inasemekana kwamba wanyakuzi hutoa kibunda kizuri na kumpatia mmoja kati ya wakaazi wa hapo ili kuanzisha moto. Moto wenyewe unapowaka basi hakuna kinachobakishwa. Hii ni kwa sababu magari ya zima moto daima dawama huchelewa kufika. Yanapofika nayo hukabiliwa na shida ya kuingia mtaani kwa ukosefu wa njia za kupitia kwani mtaa umejengwa kiholela. Wazima moto wenyewe hujikuta wamefanya kazi nusu na mara maji huwaishia.

Mioto hiyo huwamaliza watu ambao kufumba na kufumbua hujikuta hawana mbele wala nyuma. Wao hupoteza kila kitu chao. Si nguo si fanicha tu bali wengine hata na akiba yao ambayo huwa wameificha huko. Mara nyingine hata pia roho hupotea maana moto hutokea usiku wa manane watu huwa wamelala fofofo.

31. Mioto hutokea sana ____
   A. nchini Kenya
   B. katika mitaa ya mabanda
   C. jijini Nairobi
   D. katika miji mikuu

32. Wanyakuzi ni watu wenye sifa mbaya katika jamii. Nani kati ya hawa pia ana sifa mbaya katika jamii yake?
   A. Mzalendo    B. Barakala
   C. Mkereketwa    D. Mlalahoi

33. Ina walakini, ina maana gani?
   A. Ina upungufu    B. Inashtua
   C. Ina shaka    D. Ina nguvu

34. Sababu ya kutokea hii mioto huenda ikawa ni ____
   A. unyakuzi wa ardhi
   B. dharau la wakaazi
   C. stovu kusahauliwa
   D. kuchelewa kwa wazima moto

35. Njia ambayo wanyakuzi hutumia ni ____
   A. kutupa moto mtaani
   B. kuacha stovu ikiwaka
   C. kutumia mmoja wa wakaazi
   D. kumwaga mafuta na kuwasha

36. Sababu alizozitaja mwandishi zinazofanya moto kumaliza kila kitu ni ____
   A. 2    B. 4
   C. 5    D. 3

37. Kinyume cha 'kiholela' ni kwa ____
   A. msongamano    B. urembo
   C. nidhamu    D. umaridadi

38. Neno jingine badala ya fanicha ni ____
   A. masafa    B. vyombo
   C. makalio    D. samani

39. Shida kubwa inayowakabili wazima moto hawa ni ____
   A. maji    B. vifaa
   C. njia    D. magari

40. Sababu ya roho kupotea ni ____
   A. moto huwa na makali sana
   B. milango huwa imefungwa
   C. watu huwa kwenye usingizi
   D. watu huwa wamelewa

**_Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali._**

Manufaa ya miti ni mengi, hasa kwa binadamu na wanyama pia. Lakini jambo la kustaajabisha ni huyu mwanadamu ambaye hufaidika zaidi akakatikiwa kukata miti ovyoovyo kwa ajili ya masilahi yake yeye mtu mmoja binafsi.

Miti hutupa vyakula. Sisi hupata vyakula kwa njia ya matunda, mboga na hata mizizi kama vile mihogo. Ipo miti inayotupatia dawa. Mti maarafu sana ni ule mwarubaini ambao unasemekana unatibu magonjwa arobaini. Mnaraha hutibu pumu, mlama ni dawa ya sumu ya nyoka, mkarafuu ni kwa jino au tumbo linapouma na kuna mshubiri unaotibu maradhi kadhaa. Kuna pia miti ya manukato kama vile muasumini, mwaridi, mkadi, mkilua na mlangi langi. Miti hutupa vivuli na kutupatia mbao ambazo tunazitumia kwa manufaa mbalimbali. Wanyama nao hufaidika kwa namna zao. Wako wanaoishi wakitegemea miti kama chakula chao kama akina ndovu na twiga. Wako wanaoishi mitini na kuifanya ni majumba au maficho yao kama akina chui, nyoka na nyani. Ndege na wadudu nao pia hufaidika.

Miti inapokatwa nasi ni wazi kwamba tanataka kujinyima neema zote hizi mbali na kukimbiza mvua. Atakayeumia zaidi mwishoni ni mwanadamu maana bila ya miti na mimea maisha yake yako gizani.

41. Binadamu hukata miti kwa sababu ____
   A. miti humletea mashaka
   B. ya manufaa yake pekee
   C. ya kuwakimbiza nyoka
   D. ya kuwaondoa nyani mtaani

42. Mti wenye manufaa zaidi kwa dawa ni ____
   A. mshubiri  B. mnaraha
   C. mwarubaini  D. mkarafuu

43. Mti unaotusaidia kuondoa au kupunguza sumu ya nyoka ni ____
   A. mnaraha  B. mlama
   C. mkarafuu  D. Mshubiri

44. Miti ya manukato ni aina ya miti ambayo ____
   A. inanukia  B. inanuka
   C. inakata  D. inakatiza

45. Wanyama waliotajwa katika makala haya ni ____
   A. 7  B. 3
   C. 6  D. 5

46. Sentensi ipi si sahihi kulingana na makala haya?
   A. Wanyama hutumia miti ili kujificha
   B. Wanadamu hupata faida zaidi kuliko wanyama
   C. Mvua hunyesha hata miti ikikosekana
   D. Mafuta mazuri hupatikana kwa kutumia baadhi ya miti

47. Mwandishi hakutueleza jinsi ____ anavyofaidika kwa miti
   A. twiga  B. nyoka
   C. nyani  D. ndege

48. Kwa mujibu wa makala haya, ukataji miti ____
   A. utaleta giza
   B. wanyama watadhurika zaidi
   C. utafanya kukosa mvua
   D. unafaida na hasara

49. Malangi langi ni aina ya miti ____
   A. ya manukato
   B. inayotupa vivuli
   C. yenye kutupa dawa
   D. ya kutupa chakula

50. Wanyama hufaidika kwa namna ngapi kwa mujibu wa makala haya?
   A. 3  B. 4
   C. 5  D. 6